



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE



Kumb.Na.BHDC/S1/27/76

18/05/2023

**YAH: TANGAZO LA KAZI.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe amepokea kibali cha kuajiri kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb.Na.FA.97/228/01 "TEMP"/06 cha tarehe 06 April, 2023 kilichoruhusu nafasi 01 kwa utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya Ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hivyo, ninawatangazia na kuwakaribisha Wananchi wote na Watanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa kama ifuatavyo;

**MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II NAFASI 1 (RECORD MANAGEMENT ASSISTANT II)**

**1.01 Sifa za Mwombaji.**

- I. Awe amehitimu kidato cha IV
- II. Awe na Astashahada (NTA LEVEL 5) katika fani ya Urasimu ramani (Cartography) au (genoinfomatics), Sheria, Afya au Masjala kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye ujuzi wa Kompyuta.

**1.02. Kazi na Majukumu ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II.**

- I. Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista. (*Incoming correspondence Register*).
- II. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi. (*Outgoing correspondence Register*).
- III. Kusambaza majalada kwa watendaji (Action officers)
- IV. Kupokea majalada yanayo rudi masjala toka kwa Watendaji.
- V. Kutafuta kumbukumbu, nyaraka, Majalada yanayohitajika na watendaji.
- VI. Kurudisha majalada kwenye Shubaka/kabati la majalada au mahali pengine yanapohifadhiwa.

VII. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi.

### **MSAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya serikali yaani **TGS B** kwa mwezi.

### **MASHARITI YA JUMLA.**

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyewe umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
  - II. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
  - III. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (wasifu) yanayojitosheleza (Detail CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu wa kuaminika.
  - IV. Maombi yote yaambatane na vyeti vya elimu na taaluma yaani nakala ya cheti cha Kidato cha nne au sita vyeti kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kupotea au kudondoka. Picha moja ya "passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
  - V. Testmonial, "**provisional Results**" , "**Statement of results**", hati matokeo za kidato cha nne na sita ( FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
  - VI. Waombaji walio staafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama anakibali kutoka kwa Katibu Mkuu.
  - VII. Waombaji Kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **wasiombe** na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka na CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010.
  - VIII. Uwasilishaji wa taarifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.
  - IX. Kila mwombaji ahakikishe ana kitambulisho cha Taifa cha Uraia (NIDA).
  - X. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 24/05/2023 saa 9.30 Alasiri.**
- XI. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kuititia anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe,  
S.L.P 443,  
BUHIGWE.**

Imetolewa na,



Essau H. Ngoloka

**MKURUNGEZI MTENDAJI (W)**

